# Naibu Waziri ataka uandaliwe mkakati shirikishi wa chanjo

Na MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, ameagiza kuandaliwa kwa mkakati shirikishi wa kupeleka chanjo kwa wafugaji kuanzia Februari, mwakani, kupitia programu za chanjo ya magonjwa muhimu zitakazosimamiwa na wizara.

Agizo hilo, alilitoa mwishoni mwa wiki iliyopita, wakati akifunga kikao cha 38 cha Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania (TVA) kilichofanyika mkoani Arusha, kuanzia Desemba 10 hadi 12, mwaka huu.

Pia, alizindua mchanganyiko wa chanjo tatu kwa ajili ya kuku kwenye magonjwa ya mdondo, ndui na mafua na kuagiza kuanzishwa kwa uchanjaji wa mifugo, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha wizara inasimamia chanjo ya magonjwa yote ifikapo mwaka 2022.

"Hizi programu zitasimamiwa na wizara,siyo kuiachia halmashauri kwa kuwa hawana uwezo wa kutekeleza majukumu

> **Hizi programu zitasimamiwa na wizara,siyo kuiachia halmashauri kwa kuwa hawana uwezo wa kutekeleza majukumu haya muhimu.**
>
> Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul

haya muhimu, hivyo kwa kuwa wizara imeshatayarisha kalenda ya chanjo na bei elekezi, licha ya mapungufu machache yaliyopo, ninamuelekeza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, aende kuandaa mkakati shirikishi na kupeleka chanjo kwa wafugaji kuanzia Februari, mwakani," alisema.

Aidha, Naibu Waziri, alisema kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya mwaka 2003, serikali inapaswa kuhakikisha ina madaktari wa mifugo katika mikoa na halmashauri, kwa kutambua kuwa kwa muda mrefu kumekuwepo na ukosefu wa madaktari wa mifugo kwa mikoa 10 na halmashauri 77.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na halmashauri husika, zitawasilisha mapendekezo ya ikama ya watumishi kwa utumishi kwa ajili ya kuingizwa kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022, lengo likiwa ni kuhakikisha watumishi wanaajiriwa ili kusimamia vizuri tasnia ya wanyama.

Alisema kwa kutambua kilio kikubwa cha watumishi waliojiendeleza kimasomo, ambao hawatambuliwi na mfumo wa utumishi kwa kuwa wizara haijaanisha sifa ya mafunzo hitajiwa kwa watumishi wa sekta ya mifugo, tathmini itafanyika ili wizara iainishe mafunzo hitajika kwa watumishi wa kada mbalimbali na kuwasilisha utumishi ili walio na sifa hitajika wafanyiwe marekebisho katika mfumo wa kiutumishi na kuwaongezea ari ya kufanya kazi.

Kwa kuzingatia changamoto zilizopo katika sekta ya mifugo nchini, Naibu Waziri, alisema atamshauri Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kuunda kikosi kazi kishirikishi kwa ajili ya kushauri wizara katika masuala muhimu.

Aidha, alimtaka Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania, kuandaa andiko ili liwasilishwe kwa Waziri Ndaki kwa ajili ya kupata ridhaa yake.

Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania (TVA), anayemaliza muda wake, Profesa Dominick Kambarage, alisema mfumo wa kusimamia watumishi na sekta ya mifugo ni muhimu kuhakikiwa ili kuimarisha sekta hiyo, ambapo mwaka 2019, TVA na TAMISEMI walianzisha mazungumzo kwa kina namna ya kusimamia sekta na watumishi.

Maelekezo>> Simamieni sheria...

# Dk. Mpango aziag... kutoa ushirikiano ...

ROSE MWEKO Na EDITHA EDWARD, Geita

SERIKALI imeuagiza Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kukamilisha mfumo wa kielekroniki wa kushughulikia misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Akizungumza mwishoni mwa wiki iliyopita, katika ufunguzi wa mkutano wa 15 wa Baraza la Wafanyakazi wa TANROADS, Waziri wa Fedha, Dk. Philip Mpango, alisema hatua hiyo itapunguza uhimilishaji na uchapaji wa hati ya msamaha katika miradi mikubwa inayoendelea nchini na kuwasaidia wakandarasi wazawa waweze kushiriki katika ujenzi miradi mikubwa ya kimkakati.

Pia, aliagiza kitengo cha uthamini cha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na idara zingine, wakae kuten... kiutendaji wa... ya kiuthamini... shughuli za uje... barabara.

"Kumekuwa... linapotokea ... mali pindi u... unapoendelea... wananchi kuv... aina ya utham...

Aidha, D... TANROADS, ... sheria ya m... kanuni zake k... manunuzi ya... kuhakikisha w... mikataba mib...

Mkurugen... Mhandisi Pa... mkutano w... Wafanyakazi, ... mambo mbal... wafanyakazi.

Kadhalika, ...

UJENZI



MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo (wa tatu ... Tanzania (TRA), Hamna Kalunga (kulia), kuhusu maen... mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu)

# Mamlaka ya Majisafi Mbeya yaomba ...

Na SOLOMON MWANSELE, Mbeya

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya, imemuomba Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk.Tulia Ackson (CCM), kusaidia ilipwe madeni sugu inayodai taasisi mbalimbali, zikiwemo za umma, yanayofikia zaidi ya sh. bilioni 2.3.

Imesema kulipwa kwa madeni hayo, kutaiwezesha mamlaka hiyo kutekeleza miradi mbalimbali ya maji, ili kuiwezesha jiji la Mbeya kuwa na maji ya uhakika kwa saa 24 kwa siku.

Ombi hilo limetolewa na Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Mhandisi Mengo Ndele, mbele ya mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Naibu Spika wa Bunge, Dk.Tulia, kwenye kikao chake na watumishi wa mamlaka hiyo, jijini humo.

Alisema ... mbalimbali, ... wa kusaidia... hizo na ofisi... sh. 2,363,21... yamehifadhi...

Mhandisi... wa madeni... kunasababis... mamlaka hiy... 100, hivyo k... magumu.

"Lakini h... miradi ming... tulipanga ili... jiji hili la Mb... alisema Mh...

Alitaja ... kidogo cha ... mahitaji kwa...

Scanned with CamScanner

**Sh. 2,000>> Bei ya kilo moja ya punda inayouzwa kiwandani**

# Kiwanda chasitisha uzalishaji nyama ya punda, wafanyabiashara wahaha

**Na CHIBURA MAKORONGO,** *Shinyanga*

WAFANYABIASHARA wa punda nchini wanaokiuzia kiwanda cha machinjio ya bidhaa hiyo cha Fanghua, kilichopo Shinyanga, wamejikuta katika sintofahamu baada ya kukwama kwa siku zaidi 40, kutokana na kiwanda hicho kushindwa kupokea punda kwa madai ya kusitisha uzalishaji kwa muda usiojulikana.

Wafanyabiashara hao, ambao wako kwenye vikundi zaidi ya 100, walifika mkoani Shinyanga na punda zaidi ya 2,000, wakiwapeleka kiwandani hapo tangu Oktoba 24, mwaka huu, lakini walishindwa kuwauza baada ya uongozi wa kiwanda kuwaambia hawachukui tena bidhaa hiyo.

Wakizungumza na waandishi wa habari nje kidogo ya mji wa Shinyanga, walikowahifadhi punda hao, wafanyabiashara hao waliiomba serikali kuingilia kati kuwanusuru kwa mateso wanayopitia kwa zaidi ya siku 40.

Mfanyabiashara Selina Amon, kutoka mkoani Manyara, alisema baada ya kiwanda hicho kufungwa, wanyama hao wamekosa malisho na kusababisha baadhi ya punda kufa kwa njaa.

"Tuna mikopo, tunaishi kwa tabu, watoto shuleni wamerudishwa na familia zinatutegemea. Tulinunua punda tukaleta, kiwanda kimesema hawanunui tena, sasa tunashindwa tufanyeje, tuko ugenini hapa kwa siku 40 sasa, kila siku tunababaishwa, mara subirini kidogo," alisema.

Yohana Lucas, ambaye ni mfanyabiashara kutoka Manyoni, mkoani Singida, alieleza kuwa baada ya kukosa msaada, waliamua kwenda Dodoma, ambako pia hawakupata maelezo yanayojitosheleza.

"Tunawaomba viongozi watusaidie, tunamuomba Rais wetu atusaidie tuendelee kufanya biashara hii, ambayo ilikuwa mkombozi kwetu," alieleza.

Akizungumza kwa njia ya simu kueleza sababu za kiwanda kusitisha kupokea bidhaa hiyo, Meneja wa kiwanda hicho, Alice Mingyang Yan, alisema wamefanya hivyo tangu Oktoba 24, mwaka huu, kutokana na mamlaka za serikali kutojali hoja zao wanazoziwasilisha.

Alibainisha kuwa kwa sasa, anaendelea kulifuatilia suala hilo kwa mamlaka za serikali ili kupata muafaka, warejeshe shughuli za uzalishaji huku akiwataka wafanyabiashara hao wa punda kupeleka kilio chao kwa serikali.

Akitolea ufafanuzi suala hilo, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema uongozi wa wilaya na mkoa wa Shinyanga, wanalifahamu tatizo hilo na kwamba, tayari uongozi wa kiwanda cha Fanghua, umechukua hatua za kulifuatilia ngazi za juu.

Mboneko, alisisitiza kuwa mwenye kiwanda alitakiwa awajulishe wafanyabiashara mapema ili wasipate changamoto hiyo, huku akibainisha kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na EPZA, wanalishughulikia na matumaini yake ni kwamba litapata ufumbuzi mapema.

Kiwanda cha Fanghua, ndicho pekee cha machinjio ya punda nchini, ambapo wafanyabaishara kutoka mikoa mbalimbali nchini, ikiwemo Mbeya, Dodoma na Manyara, hununua mifugo hiyo kwenye minada na kukiuzia kiwanda hicho, kulingana na uzito wa kila punda. Kilo moja ya nyama ya punda ni sh 2,000.

ILANI YA CCM IMETEKELEZWA

Scanned with CamScanner

Monday 14 December 2020

The Guardian

*

# NARCO vaccinates cattle against contagious disease

By Guardian Reporter, Dodoma

THE National Ranching Company Limited (NARCO) has started vaccination against contagious bovine caprine pleuropneumonia (CBPP), treating 9,237 head of cattle at the Kongwa based farm.

The move is among the directives issued by the Minister for Livestock and Fisheries, Mashimba Ndaki in December, this year.

NARCO's acting general manager, Masele Shilagi said this in a speech to the minister when he visited NARCO yesterday, adding that the vaccination exercise took about ten hours.

Shilagi said after the launch of the exercise it will be rolled out to other livestock owned by private investors within the NARCO farm: "We have alerted the Tanzania Veterinary Laboratory Agency (TVLA) in efforts to get vaccine doze for 6800 livestock still left in 13 ranches and the vaccinations will start next week," he said .

The NARCO boss appealed to livestock keepers neighbouring Kongwa ranch not to be worried since the government has taken positive steps towards fighting against the disease.

On his part, minister Ndaki who made an impromptu visit at the ranch in Kongwa after the out break of the disease called on the acting NARCO manger to ensure all cows were vaccinated against the disease.

He said, "Make sure all cows in the national ranches are vaccinated against this deadly disease".

CBPP is caused by the bacteria mycoplasma mycoides species. As the name suggests, CBPP mainly affects the lungs and the membranes that line the thoracic cavity resulting in fever and respiratory distress such as laboured or rapid breathing, cough and nasal discharge.

About 15 per cent of infected animals die in endemic areas and up to 70 per cent when introduced into naive herds, lactation loss is up to 90 per cent.

It has a devastating impact on livestock owners. It leads to reduced incomes through lower animal productivity, trade restrictions imposed on live cattle by disease-free countries, increased costs for veterinary services, and death.

CBPP is currently considered to be the most important bacterial livestock disease in sub-Saharan Africa. It currently affects over 20 countries in Africa and is suspected to be present in Asia.

The economic implications of CBPP are difficult to estimate since diagnostic surveys for many regions in sub-Saharan Africa are absent, but preliminary estimated costs of at least USD 100 million per year in Africa, approximately USD 6.1 million per country are likely.

Scanned with CamScanner

Jumatatu – MAJIRA – 14/12/2020

# Serikali yaja na mkakati wa chanjo za magonjwa ya mifugo

**Na Edward Kondela, Arusha**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul ameagiza kuandaliwa kwa mkakati shirikishi wa kupeleka chanjo kwa wafugaji kuanzia mwezi Februari Mwaka 2021 kupitia programu za chanjo ya magonjwa muhimu zitakazosimamiwa na wizara.

Akizungumza wakati akifunga kikao cha 38 cha Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania (TVA) kilichofanyika Mkoani Arusha ambapo pia alizindua mchanganyiko wa chanjo tatu kwa ajili ya kuku kwenye magonjwa ya mdondo, ndui na mafua ameagiza kuanzishwa kwa uchanjaji wa mifugo ikiwa na lengo kuu la kuhakikisha wizara inasimamia chanjo ya magonjwa yote ifikapo Mwaka 2022.

"Hizi programu zitasimamiwa na wizara na siyo kuiachia halmashauri kwani wao hawana uwezo wa kutekeleza majukumu haya muhimu, hivyo kwa kuwa wizara imeshatayarisha kalenda ya chanjo na bei elekezi licha ya mapungufu machache yaliyopo ninamuelekeza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo aende na aandae mkakati shirikishi na kupekeleka chanjo kwa wafugaji kuanzia mwezi Februari, mwaka 2021," alisema Gekul.

Aidha, Naibu Waziri Gekul alisema kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya Mwaka 2003 serikali inapaswa kuhakikisha ina madaktari wa mifugo katika mikoa na halmashauri kwa kutambua kuwa kwa muda mrefu kumekuwepo na ukosefu wa madaktari wa mifugo kwa mikoa 10 na halmashauri 77 Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na halmashauri husika itawasilisha mapendekezo ya ikama ya watumishi kwa Utumishi kwa ajili ya kuingizwa kwenye bajeti ya mwaka 2012/2022, lengo ikiwa ni kuhakikisha watumishi hawa wanaajiriwa ili kusimamia vizuri tasnia ya wanyama.

Pia, Gekul alisema kwa kutambua kilio kikubwa cha watumishi waliojiendeleza kimasomo ambao hawatambuliwi na mfumo wa utumishi kwa kuwa wizara hajaainisha sifa ya mafunzo hitajiwa kwa watumishi wa sekta ya mifugo, tathmini itafanyika ili wizara iainishe mafunzo hitajiwa kwa watumishi wa kada mbalimbali na kuwasilisha utumishi na hivyo wale walio na sifa hitajiwa kufanyiwa marekebisho katika mfumo wa kiutumishi ili kuwaongezea ari ya kufanya kazi.

Kwa kuzingatia changamoto zilizopo katika Sekta ya Mifugo nchini Naibu Waziri Gekul amesema atamshauri Waziri wa Mifugo na Uvui, Mashimba Ndaki kuunda kikosi kazi kishirikishi kwa ajili ya kuishauri wizara katika masuala muhimu na kumtaka Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Msajili wa Baraza la Vetarinari Tanzania, kuandaa andiko ili liwasilishwe kwa Waziri Ndaki kwa ajili ya kupata ridhaa yake.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania (TVA) anayemaliza muda wake, Prof. Dominick Kambarage amesema mfumo wa kusimamia watumishi na Sekta ya Mifugo ni muhimu kuhakikiwa ili kuimarisha sekta hiyo ambapo Mwaka 2019 TVA na TAMISEMI walianzisha mazungumzo kwa kina namna ya kusimamia sekta na watumishi.

Naye Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania, Dkt. Bedan Masuruli akizungumza kando ya kikao cha 38 cha Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania (TVA), amesema baraza limejadili pia maadili kwa wataalam mbalimbali wa mifugo ambao wameshindwa kutoa taarifa za magonjwa kwa idara ya huduma za mifugo kila wiki na kila mwezi, hivyo kulazimika kutoa onyo kali kwa wataalamu 9 juu ya utoaji wa taarifa.

"Tarehe 9 Desemba Mwaka 2020 baraza liliitisha kikao cha dharula kujadili maadili na kushuhudia karibu asilimia 44 ya wataalamu hawatoi taarifa za magonjwa ya mifugo ambapo katika wilaya 184, wataalamu 78 walikuwa wahatoi taarifa lakini baada ya kufanya mahojiano ya awali, wataalamu 34 walibakia kutotoa taarifa ambapo 19 walifika kwenye kikao na walipohojiwa wataalamu 9 walionekana hawana ushahidi wamepewa onyo kali na kuhakikisha katika mwaka mmoja hawakosi kabisa kutoa taarifa za magonjwa ya mifugo kila wiki na kila mwezi," alifafanua Dkt. Masuruli.

JUMATATU – MAJIRA – 14/12/2020

Scanned with CamScanner

aalumu kwa ajili ya kilimo, mifugo

# vasilisha hoja binafsi u mikataba ya ardhi

hata wawakilishi wa rais (mkuu a wilaya na mkuu wa mkoa), ituruhusiwi kuipitia, ni lazima iangalie kwa jicho la tatu kwa maslahi wananchi wetu," alisema Mafuwe.

Akizungumzia kuhusiana na ha ya upatikanaji wa maji, Mafuwe sema tangu alipochaguliwa siku zilizopita, tayari ameshafanya zungumzo na uongozi wa Jiji la sha, kuona namna watakavyoweza pata maji kutoka kwao na kuyapeleka ika ukanda wa tambarare kutokana maeneo hayo kuwa karibu.

Alisema mbali na kuongea na gozi wa jiji hilo, pia amewasiliana Wizara ya Maji, ambapo nemhakikishia watafika jimboni io kuona namna watakavyoweza ata vyanzo vingine vya maji ili sheleza wakazi wa Jimbo la Hai.

Kuna watu wanaitwa bodi za imia maji, hawa wamekuwa toza gharama kubwa kiasi nba, hata mtu anashindwa ganishiwa huduma ya maji. io, mimi binafsi nilitaka ganishiwa maji, lakini gharama ni shilingi 720,000 na wanataka vifaa wakanunue wao, kwanini ruhusu mteja akanunue nyewe kwa bei ya soko?" Alihoji.

Mbunge huyo alivitaja vitu vingine avyo tayari ameshaanza kuchukua hatua ni huduma ya matibabu kwa wazee, ambapo wataanza kunufaika na huduma ya matibabu bure baada ya usajili kukamilika.

Kwa mujibu wa Mafuwe, tayari upembuzi umeshafanyika na alishafanya mazungumzo na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na kuona namna ya kufanya mchakato huo kwa ufanisi zaidi na kuwafikia wazee wengi kama ilivyo kipaumbele na dira ya serikali ya awamu ya tano.

Katika hatua nyingine, mbunge huyo alifanya kikao kazi kikichowakutanisha Taasisi ya Kupima Viwango vya Udongo (TARI), Taasisi ya Kilimo Tengeru, Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TACRI), madiwani wa Halmashauri ya Hai na watumishi wengine.

Alisema licha ya kwamba jimbo hilo lina changamoto lukuki, ameona ni vema akaanza na kilimo kwa kuwa ni sekta mtambuka na ndiyo inayobeba matumaini ya wengi.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Hai, Kumotola Kumotola, alisema mbunge huyo kwa kipindi kifupi, amefanya mambo mengi, hivyo watumishi wa halmashauri wanatakiwa kuonyesha ubunifu katika utendaji wao ili kuleta maendeleo yaliyokosekana kwa kipindi kirefu.



**NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Mary Maganga, akihutubia Mahafali ya 18 ya Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi za Singida, Mwanza na Kigoma, yaliyofanyika Singida, juzi. Kutoka kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo nchini, Profesa Carolyne Nombo na Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Utawala, Dk. Momole Kasambala.**

## CCM yaagiza migogoro wakulima, wafugaji itatuliwe haraka

**Na SALVATORY NTANDU, Msalala**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Shinyanga, kimewataka madiwani wa Halmashauri ya Msalala Wilayani Kahama, kuhakikisha wanatatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji katika maeneo yao.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Katibu wa CCM, Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa, alipozungumza na madiwani hao, baada ya kuapishwa kuanza kutekeleza majukumu yao ya kuwatumikia wananchi.

Alisema wakati umefika kwa kila diwani kuhakikisha anatatua migogoro katika eneo lake la utawala, hususan ya wafugaji na wakulima, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Msalala, kwa kuwatengea maeneo maalumu kwa ajili ya kilimo na mifugo.

"Serikali ya CCM imejipanga kutatua kero zote za wananchi wanyonge, hivyo hakikisheni mnakuwa sehemu ya kutatua matatizo yao. Tumieni uwezo wenu kuhakikisha wananchi wanaipenda serikali yao na kuchangia shughuli za maendeleo kama vile ujenzi wa madarasa na miundombinu mbalimbali," alisema Magesa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala, Mibako Mabubu, alisema wameyapokea maagizo hayo na watahakikisha wanayatekeleza kwa vitendo.

> **"Serikali ya CCM imejipanga kutatua kero zote za wananchi wanyonge, hivyo hakikisheni mnakuwa sehemu ya kutatua matatizo yao. Tumieni uwezo wenu kuhakikisha wananchi wanaipenda serikali yao na kuchangia shughuli za maendeleo.**
>
> Katibu wa CCM, Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa

Aliwataka madiwani kuhakikisha wanawashirikisha wananchi katika utatuzi wa matatizo mbalimbali katika maeneo yao ya utawala.

Mbunge wa Jimbo la Msalala, Iddi Kasimu, aliwataka madiwani hao kuwa wamoja na kuvunja makundi yaliyokuwepo wakati wa uchaguzi mkuu, badala yake waelekeze nguvu zao katika kutetea wananchi ili kuhakikisha jimbo hilo linasonga mbele katika maendeleo.

Scanned with CamScanner